LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar es Salaam, Tanzania
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

# TAMKO KUHUSU HALI YA LOLIONDO NA NGORONGORO
**TAREHE 30/06/2022**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika lisilokuwa la kiserikali lisilofungamana na upande wowote wala kutengeneza faida. Kazi kubwa ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kutetea, kukuza na kuendeleza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla hasa makundi ya jamii ambayo bado yamekuwa kando katika upatikanaji wa haki.

Lengo la tamko hili ni kutoa maoni, mapendezo na mtazamo wetu kuhusu zoezi linalotekelezwa na serikali katika eneo la Loliondo na Ngorongoro wilayani Ngorongoro mkoa wa Arusha.

## Eneo la Loliondo

Kama inavyofahamika, eneo la Loliondo lilianzishwa kama eneo la pori tengefu chini ya sheria ***Fauna Conservation Ordinance*** Sura 302 ya mwaka 1951 na eneo hili lilikuwa na kilometa za mraba 4000. Loliondo ilikuwa moja kati ya mapori tengefu 49 yaliyoanzishwa na sheria hiyo. Kuanzishwa kwa mapori tengefu hata hivyo haki za wananchi waishio maeneo hayo haikuondolewa na sheria. Hii ilimaanisha kwamba, shughuli zote za kibinadamu katika meeneo yaliyotangazwa kuwa pori tengefu yaliendelea bila kutatizwa na sheria. Wakati wa kuanzisha mapori tengefu, lengo kuu lilikuwa kwa ajili ya uratibu wa wanyapori katika maeneo ya watu na uwindaji.

Baada ya Operesheni Vijiji kuanza, vilianzishwa na kusajiliwa vijiji kadhaa katika eneo la Loliondo na Sale ambayo sasa yanahusika na mgogoro unaoendelea kama ifuatavyo:

**Board of Directors:**
Hon. Chief Justice (Ret'd) Barnabas A. Samatta - Chairperson, Ms. Anastazia Rugaba - Vice Chairperson,
Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Rebeca Z. Gyumi - Member,
Ms. Sophia M. Komba - Member, Dr. Abdullah H. Mohammed - Member, Ms. Josephine A. Zimba - Member,
Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki - Member

| | Jina la Kijiji | Mwaka wa Usajili wa Kijiji | Namba ya hati ya Usajili wa Kijiji | Hati ya Ardhi | Ukubwa kwa Hekta | Mwaka wa Usajili wa ardhi ya Kijiji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ololosokwan | 25/04/1978 | AR.KIJ. 404 | 7262 | 51,230 | 13/10/1990 |
| 2 | Soitsambu | 15//5/1978 | AR.KIJ. 407 | 7275 | 73,342 | 13/10/1990 |
| 3 | Oloipiri | | | 7182 | 47,100 | 13/10/1990 |
| 4 | Oloirien Mgaiduru | 8/9/1978 | AR.KIJ. 406 | | 30,340 | 13/10/1990 |
| 5 | Oloosoito/Maaloni | 26/12/1978 | AR.VC.406 | 7259 | 77,860 | 13/10/1990 |
| 6 | Arash | 8/9/1978 | AR.KIJ. 405 | 7264 | 66,800 | 13/10/1990 |

Kwa sasa, kuna jumla ya vijiji 14 ambavyo vinaathirika na hali inayoendelea katika uwekwaji wa mipaka katika eneo la Loliondo na Sale ambapo wananchi kwa maelfu wanaishi ndani ya eneo hili.

Mwaka 1992, eneo la pori tengefu la Loliondo iliwekezwa na Brigadier Mohhammed Al Ali na baadae na kampuni ya Otterlo Business Corporation (OBC)Ltd kwa shughuli zao binafsi za utalii ikiwepo uwindaji. Mahusiano ya jamii na mwekezaji kupitia kampuni ya OBC yalikuwa duni tangu mwanzo na kampuni hii ililalamikiwa kugubikwa na rushwa tangu mwanzo. Hisia za matumizi mabaya ya fedha katika kutekeleza kazi zake yalidhihirishwa na kauli ya aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mh. Hamis Kigwangalla kuwa kampuni ya OBC ilitaka kumhonga dola laki moja https://www.youtube.com/watch?v=rWGlhdMb1As ambapo alisema mtangulizi wake alihongwa dola laki mbili na kwamba kampuni hiyo inatumia fedha kwa watumishi wakuu wizara ya Maliasili na Utalii kama rushwa.

Mwaka 2009, sheria ya ***Fauna Conservation Ordinance*** ilifutwa na Sheria ya wanyamapori Na 5 ya mwaka 2009. Katika kifungu cha 16(4) ilieleza bayana kwamba, Waziri kwa kushauriana na serikali za mitaa atalazimika kupitia

mapori tengefu na kubainisha yale ambayo bado kuna sababu ya kuyaendeleza kama pori tengefu.

Kifungu cha 16(5) kiliweka bayana kuwa katika kupitia pori tengefu, Waziri ahakikishe kwamba hakuna pori tengefu litakalokuwa katika ardhi ya Kijiji. Hii inamaanisha kwamba, yaliyokuwa mapori tengefu ambayo kwa namna yeyote yanakuwa katika ardhi ya vijiji basi hayawezi kuendelezwa kama pori tengefu miezi kumi na mbili tangu kuidhinishwa kwa sheria ya wanyapori Mwaka 2009.

Mpaka sasa, miaka kumi na tatu baadae, hakujawahi kuwepo tangazo la kisheria kuidhinisha kuwa lililokuwa pori tengefu la Loliondo linaendelezwa kama pori tengefu. Pili, mpaka sasa, utaratibu wa kumega kilometa za mraba 1500 kwa nia ya kufanya eneo la pori tengefu inakiuka sheria ya wanyapori kwani inakuwa ndani ya ardhi ya vijiji hivyo kupingana na dhamira ya kifungu cha 16(5) ya sheria ya Wanyapori.

Tatu, kumekuwepo mkanganyiko wa sheria kuhusu matumizi ya baadae ya eneo la kilometa za mraba 1500 ambazo zimetangazwa kinyume cha sheria kama pori tengefu. Kumekuwa na kauli kadhaa kuwa wananchi wataendelea kuruhusiwa kutumia eneo hilo kwa makubaliano. Hata hivyo, sheria inayohusika na uanzishwaji wa pori tengefu inaelekeza bayana kuwa shughuli za binadamu ufugaji na makazi hayataruhusiwa kisheria. Hivyo ni muhimu kabla ya kuendelea na mchakato wa kuweka alama wananchi washirikishwe kwa umakini mkubwa na Serikali za mitaa ambazo ndizo zipo karibu na waanchi ziridhie kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 16(4) ya sheria ya Wanyapori ya mwaka 2009.

Vuguvugu la kutwaa ardhi na Loliondo kuwa pori tengefu na kuondoa wananchi ni la muda mrefu. Mwaka 2013, aliyekuwa Waziri **Mkuu Mizengo Pinda kupitia barua ya tarehe 30/5/2013 ya kumbukumbu namba PM/P/1/569/29** kwenda kwa Magesa Mulungo aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha alielekeza kusitishwa kwa mpango wa kutangaza eneo la kilometa za

mraba 1500 kuwa eneo la pori tengefu kwa sababu lipo chini ya ardhi ya vijiji vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria. Barua hiyo ilinakiliwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi na Waziri wa Maliasili na Utalii. Aliyewahi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jakaya Mrisho Kikwete aliwahi kukaririwa kupitia mitandao ya kijamii akieleza kuwa Serikali ya Tanzania haijawaondoa na haitawaondoa Jamii ya Kimasai katika eneo lao la asili ambalo ni eneo linalohusika na mgogoro wa sasa.

Hali iliyokuwepo wakati ule haijabadilika hata sasa na zaidi, kazi inayoendelea ya kuweka alama za mpaka katika eneo la kilometa za mraba 1500 imeleta hofu kubwa kwa wananchi, mgogoro wa kisheria na haina afya kwa ustawi wa taifa letu katika macho ya kimataifa.

Eneo linalohusika na mgogoro huu inahusika pia na kesi iliyopo katika Mahakama ya Afrika Mashariki kupitia Shauri Na 10 ya mwaka 2017. Shauri hili ilipangwa kuamuliwa tarehe 22/6/2022 kabla ya kusogezwa mbele mpaka September Mwaka huu. Mwaka 2018 Mahakama ya Afrika Mashariki kupitia shauri dogo No 15 ya mwaka 2017 ilitoa zuio la muda dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutowaondoa wananchi katika eneo lenye mgogoro mpaka maamuzi ya msingi ya Mahakama yatakapotolewa.

Siku ya tarehe 22/06/2022 siku ambayo Shauri Namba 10 ya mwaka 2017 ilipangwa kuamuliwa kabla ya kuahirishwa tarehe 17/06/2022 Waziri wa Maliasili na Utalii Pindi Chana alitangaza eneo lenye mgogoro kuwa pori tengefu kwa jina la POLOLET GAME CONTROL AREA kupitia tangazo la Serikali Na 421 ambayo ilisainiwa na Waziri siku ya tarehe 10/6/2022.

Katika kutambua umuhimu wa utawala wa sheria ni vyema kusubiri maamuzi ya Mahakama ya Afrika Mashariki kabla ya kuendelea na chochote lakini bila kujali amri ya mahakama serikali imeendelea na zoezi la kuweka mipaka ndani ya ardhi ya vijiji kinyume cha sheria na bila kushirikisha wananchi na kwa uwazi.

Kuhusu uhifadhi wa wanyamapori, ni wakati muafaka sasa Serikali kupitia sheria zinazoruhusu uwindaji wa wanyapori na kuzifuta kama njia bora kulinda wanyapori. Kuzuia uwindaji ama usafirishaji wa wanyama pori itasaidia Tanzania kuwa sehemu bora ya kufanya utalii wa picha kwa muda mrefu zaidi. Kutokana na kumbukumbu za Wizara ya Maliasili na Utalii, maeneo ambayo yanafanya utalii wa picha zinaingizia taifa fedha nyingi za kigeni na zina migogoro kidogo kulinganisha na maeneo yanayofanyika uwindaji wa wanyama.

**KUHUSU HALI YA SASA YA LOLIONDO**

Itakumbukwa tarehe 14/02/2022, Waziri Mkuu Mh. Majaliwa Khasim Majaliwa alikaririwa katika ziara yake Loliondo akisema haujaenda na malori kuwandoa wanachi kama ambavyo wengi walipata hofu hiyo. Kuanzia tarehe 6/06/2022, hali ya taharuki ilianza kutanda katika Wilaya ya Ngorongoro baada ya magari mengi ya jeshi la polisi kuingia eneo la mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro na kesho yake kuelekea eneo la Loliondo.

Taharuki hizo zilisababishwa na uhalisia kuwa maeneo hayo yamekuwa na mgogoro uliokuwa unaendelea ambayo wananchi wa maeneo yote mawili waliwasilisha mapendekezo katika ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 25/05/2022. Kuonekana kwa magari mengi ya jeshi polisi bila taarifa kwa wananchi ilileta hofu kuwa yawezekana Serikali ilikuwa inaendea kuwaondoa wananchi kwa kutumia vyombo vya ulinzi.

Hofu hiyo iliongezeka zaidi pale siku ya tarehe 9/06/2022 viongozi wengi wa kisiasa walipoitwa kwa Mkuu wa Wilaya na baadae kukamatwa ambapo hakukuwa na taarifa yoyote kuhusu walipokamatiwa mpaka walipofikishwa mahakamani tarehe 16/6/2022 kwa kosa la mauaji.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha pamoja na kusema hali katika eneo la Loliondo na shwari, alieleza kuwa askari polisi aliuawa kwa kupigwa mshale. Taarifa pia

ilisambaa kuwa wananchi zaidi ya 31 walijeruhiwa na wengine zaidi ya 20 kukamatwa.

Taarifa pia zinaeleza kuwa mzee wa makamo aitwaye Orias Oleng'iyo hajulikani alipo mpaka sasa pamoja na kuonekana na majeraha. Hali hii imelifanya taifa letu kumulikwa na vyombo mbalimbali vya habari na jamii ya kimataifa kwa jicho la ukiukwaji wa haki za binadamu. Taarifa hizi zilifuatiwa na kauli ya ofisi ya haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa na ile ya Tume ya Haki za Binadamu ya Afrika kulaani na kukemea yanayotokea Loliondo.

Wakati kuna watu wamekamatwa kwa madai ya mauaji ya polisi, hakuna polisi yeyote aliyekamatwa ama uchunguzi wowote rasmi kuhusu madai ya wananchi kupigwa risasi za moto na vyombo vya dola. Katiba ya Tanzania katika Ibara ya 12 ya Katiba ya Tanzania inaelekeza kuwa watu wote ni sawa na Ibara ya 13 inasisitiza kuwa watu wote ni sawa mbele ya sheria.

Kwa sababu sehemu kubwa ya taharuki ambayo imesambaa sehemu nyingi duniani inatokana ushiriki wa jeshi la polisi katika mgogoro unaondelea na madai ya watu zaidi ya 31 kujeruhiwa, ni muhimu kuunda tume huru inatayochunguza maswala yote yaliyotokea na yanayoendela kutokea Loliondo ili kuhakikisha kuwa Haki za Binadamu, Utawala wa sheria na Katiba ya nchi yetu inalindwa. Ni muhimu pia historia ya jambo hili likatazamwa upya kwa umakini.

Tunapendekeza Serikali ifanye hatua za makusudi kufuatilia madai ya wananchi wa Loliondo kuwa kuna idadi ya wananchi waliojeruhiwa na vyombo vya dola, mosi ili watu hao wapatiwe huduma za haraka za kibinadamu lakini pili ili kuweza kufanya uchunguzi wa kina na kuchukua hatua dhidi ya waliohusika kusababisha majeraha ama madhara mengine. Na kama kuna upotoshaji kuhusu majeruhi kama ilivyodaiwa mara nyingi wapotoshaji wachukuliwe hatua.

**ENEO LA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO**

Eneo la mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro lenye kilometa za mraba 8293 lilianzishwa chini ya sheria na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro sasa Sura ya 284 ya Sheria za Tanzania. Sheria hii katika kifungu 6 inaainisha malengo makuu matatu ya kuanzishwa kwake ambayo hujumuisha:

i. Kutambua na kuendeleza maslahi ya Jamii ya Kimasai ambayo hujishughulisha na ufugaji
ii. Uhifadhi wa ikolojia na wanyapori
iii. Utalii

Eneo hili limekuwa na historia ndefu ya mgogoro wa ulinzi wa haki za msingi za binadamu. Kwa miaka mingi, kumekuwa na mijadala ya kuhamisha wakazi wa Ngorongoro kutoka eneo hilo lakini kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya kisheria na kiutu mipango hiyo ilisitishwa na Serikali zilizopita.

Tangu mwezi wa kwanza mwaka huu, kulizuka sintofahamu katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro. Hali ilianza kuwa sio shwari pale wananchi walipowasilisha taarifa Halmashauri ya wilaya ya Ngorongoro kuwa mifogo yao wanakufa wakitumia chumvi inayotolewa na mamlaka ya hifadhi kama ilivyoelekezwa na Waziri Mkuu mwaka 2016.

Kabla ya jambo hilo kushughulikiwa vyombo vya habari vilianza kuangazia kuhusu hali ya eneo la Ngorongoro kwa kile kilichoelezwa kuwa inatokana na idadi ya watu na mifugo ndani ya eneo la hifadhi. Tarehe 9/02/2022 Bunge lilijadili jambo hili. Kwa maelekezo yako, Mamlaka ya Ngorongoro, TAWA, TANAPA waliendesha semina kwa wabunge kuhusu jambo hili. Mijadala hiyo ilileta taharuki kubwa kwa wananchi wa eneo la Ngorongoro.

Kwa nyakati kadhaa zilisambaa video na picha za mikusanyiko ya halaiki ya watu na mifugo kufungiwa bila malisho. Hii ilitokana na ukosefu wa taarifa sahihi kuhusu mpango wa Serikali juu ya eneo la Ngorongoro.

Tarehe 17/2/2022 Waziri Mkuu alikuwa kiongozi wa kwanza kuonana na sehemu ya jamii ya kimasai katika eneo hilo na kueleza nia ya Serikali kuhusu eneo la Ngorongoro. Tangu wakati huo mpaka sasa, hakuna uongozi wowote ulioendeleza maongezi hayo.

Tarehe 31/3/2022, Serikali kupitia kwa Mkurugenzi wa Halamshauri ya wilaya alielekeza kuhamishwa kwa fedha za UVIKO-19 kutoka eneo la hifadhi kwenda akaunti maalum Halmashauri ya Handeni. Mbunge wa Ngorongoro alieleza bungeni kuwa jambo hili ni sawa na kuwawekea wananchi vikwazo ili waondoke katika eneo la hifadhi.

Tarehe 28/4/2022, Msemaji wa Serikali alieleza kupitia mitandao ya kijamii kuwa Serikali imeshauriwa na wadau kuwa huduma za kijamii ndizo zinazowazuia wananchi kuondoka na ndio sababu ya fedha kuhamishwa.

Tunapendekeza kuwa huduma zote za kibinadamu ziweze kurudishwa katika eneo la Ngorongoro. Pamoja na nia ya kuhifadhi eneo la Ngorongoro ambayo ina umuhimu kiikolojia, ni muhimu wakati wote kulinda na kuheshimu haki za binadamu.

Takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii zinaonyesha zaidi ya 70% ya watalii wanaoitembelea Tanzania hutembelea mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro hivyo kuifanya roho ya utalii Tanzania. Mwezi wa nne, Rais wa Tanzania Mh. Samia Suluhu Hassan alizindua Filamu ya ***Royal Tour*** kama sehemu ya kuitangaza Tanzania kimataifa. Jambo hili lisipowekewa umakini mkubwa bure, linaweza kufanya juhudi za Rais kuitangaza utalii Tanzania isiwe na manufaa hasa mgogoro huu unapoangaziwa katika vyombo vya kimataifa katika eneo ambalo ndio linajulikana zaidi kiutalii.

Tunapendekeza juhudi za makusudi zifanyike kurudisha imani ya jamii zinazoishi katika hifadhi ya Ngorongoro katika mchakato huu

Kwa ujumla, katika wilaya ya Ngorongoro yenye kilometa za Mraba 14,036, Serikali inakusudia kutwaa zaidi ya kilometa za mraba takriban 12,000. Tarehe 22/06/2022, Waziri wa Maliasili alitangaza nia ya Serikali kupitia Sheria ya Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kwa nia ya kuhalalisha kuondolewa kwa wananchi wanaoishi katika eneo hili. Kama ilivyo eneo la Loliondo, hakuna ushirikishwaji wa kuridhisha unaofanywa kwa wananchi ambao ni waathirika wakubwa wa michakato inayoendeela. Itakumbukwa kuwa jamii ya kimasai ambayo sasa wanaishi eneo la Ngorongoro waliondolewa katika mbuga ya sasa ya Serengeti na hivyo kupoteza kilometa za mraba 14,763 ambayo ni eneo muhimu kwa malisho nyakati za kiangazi hasa baada ya wanyama wahamao kurudi eneo la Masai Mara nchini Kenya.

## MAPENDEKEZO YA JUMLA

### Eneo la Loliondo

Kutokana na hali ya sasa ya Loliondo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapendekeza mambo yafuatayo

1. Serikali ifute pori tengefu lililotangazwa kwa jina la POLOLET GAME CONTROL AREA kwa sababu uanzishwaji wake haukuzingatia sheria za nchi ikiwemo ushirikishwaji wa kutosha wa wananchi, kutwaa ardhi ya vijiji kinyume cha sheria, pamoja na kukiuka amri ya Mahakama ya Africa Mashariki kwenye shauri dogo Na 15/2017 iliyotolewa mwaka 2018.
2. Serikali iwaondoe askari na vyombo vya ulinzi katika eneo hilo vilivyohusika na uwekwaji wa mipaka katika eneo lenye mgogoro na kuendelea kuleta taharuki kwa jamii.
3. Iundwe tume huru itakayochunguza maswahibu yaliyotokea kati ya polisi na wananchi huko Loliondo pamoja na kutafuta kiini cha mgogoro wa Loliondo. Tume hiyo ishirikishe pande zote na isiongozwe na Jeshi la Polisi, wala wizara ya Maliasili na Utalii. Kwani kutakuwa na mgongano wa maslahi.
4. Serikali kupitia uongozi wa juu utoe hakikisho la usalama kwa wananchi wanaosadikika kuwa na majeraha kuwa huru kupata huduma za afya bila hofu ya kukamatwa. Hii iende sambamba na kutoa hakikisho kwa

makundi ya raia yaliyokimbilia kutafuta hifadhi nchin jirani kurudi kuendelea na shughuli zao.

5. Uchunguzi wa haraka ufanyike kuhusu madai ya mzee mmoja aliyefahamika kwa jina la Orias Oleng'iyo ambaye anadaiwa hajulikani alipo pamoja na madai ya kuwa na majeraha.

**Eneo la Ngorongoro**

1. Serikali irejeshe huduma zote za kijamii ikiwemo kuruhusu kuendelezwa kwa miradi ya afya, elimu, maji pamoja na mengine ndani ya eneo la Ngorongoro kwani hii inapingana na dhana kwamba wananchi wanahama kwa hiari.
2. Serikali ihakikishe kuwa nia yake ya kushawishi wananchi wenye nia ya kuhamia eneo lililotengwa na Serikali haiathiri haki za wananchi wasioridhia kuondoka katika eneo la Ngorongoro.
3. Serikali ichunguze madai ya Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kuwalenga kwa makusudi jamii ya kimasai ikiwemo uhamisho wa wafanyakazi wenye asili ya kimasai kuhamishwa kunakoashiria kuwa na mahusiano na asili yao.
4. Serikali iridhie kuundwa kwa Tume huru itakayochunguza madai ya mifugo kupewa sumu pamoja na ukiukwaji mwingine wa Haki za Binadamu ndani ya neo la Ngorongoro ikiwemo kuwalenga raia kutokana na asili zao
5. Mpango wa Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa nia ya kuhalalisha kuondolewa kwa wananchi isitishwe.

Tunatanguliza shukrani zetu za dhati

**IMETOLEWA NA;**

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (LHRC)**

**ANNA HENGA**

**MKURUGENZI MTENDAJI**